are aware that some embrace spiritual services as well as life tan. Child care is everyone's role for children," she said.

Daily News page 05 Tuesday 21 May, 2024.

# Govt reminds solicitors to stick to professional ethics

**From DEOGRATIAS KISHOMBO in Arusha**

THE government has urged public solicitors to maintain high level of integrity and trust in order to help the government in conflicts related legal matters.

Deputy Minister for Constitutional and Legal Affairs Jumanne Sagini made the call during the opening of a three-day capacity building seminar for public solicitors in Arusha yesterday.

He said public solicitors were crucial in supporting the government in conflict resolutions, including conflicts between the government and investors.

"You are the engine in supporting the government on legal matters. Since you are the ones who help the government, you need to be proactive and maintain high level of integrity," he said.

He said the government is implementing various strategic projects, insisting on the need for solicitors to help the government in all legal matters especially those related to investments.

Tanzania is implementing a number of strategic projects in various areas including transport infrastructure, mining, oil and gas.

"You need to make sure that the government does not lose cases on important issues, especially investment contracts. The government has invested a lot in development projects, so it's your responsibility to maintain the country's interests," he said.

He said they ought to mediate before matters are taken to courts, saying that taking the government to court was expensive and time consuming.

"You are the engine in supporting the government on legal matters. Since you are the ones who help the government, you need to be proactive and maintain high level of integrity."

On his part, Solicitor General Dr Boniphace Luhende said the seminar was important to public solicitors because it gives them opportunity to reflect and share experiences.

He said as of April this year, his office had already supported the government in solving about 7,813 claims brought against the government. He said about 7,798 were local and 15 claims were from abroad.

Dk Luhende also disclosed that from July last year to April this year, the Office of the Solicitor General (OSG) successfully mediated and solved claims brought against the government worth 1.5tri/-.

"The government has won claims worth 1.5tri/- resulted from 7,813 claims," he said.

He however, said that OSG was continuing improving its Case Inventory Management Information System -CIMS, saying that the system has helped a lot in justice delivery.

"We are moving according to the current situation. We need to go with the speed of technology. We need to support our solicitors to be high professional public solicitors" he said

# Serikali yashinda mashauri 15, yaokoa tril.1.5/-

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKILI Mkuu wa Serikali, Dk.Boniphace Luhende amesema ofisi hiyo imeokoa Sh.trilioni 1.5 baada ya kushinda mashauri 15 ya usuluhishi kati ya 19 yaliyokuwa yamefunguliwa ndani na nje ya nchi, katika kipindi cha Julai mwaka jana hadi Aprili mwaka huu.

Amesema kati ya mashauri ya madai 7,813 yaliyoendeshwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuanzia Julai 2023 hadi Aprili 2024, mashauri 762 yalimalizika, ambapo mashauri 743 yenye thamani ya Sh.bilioni 406.4 yalimalizika kwa serikali kupata ushindi.

Aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati wa mafunzo ya siku tatu ya mawakili wa serikali yaliyokuwa na kaulimbiu isemayo 'Uendeshaji wa mashauri ya serikali wajibu wa majukumu ya mawakili wa serikali' yaliyoenda sanjari na uzinduzi wa nembo itakayotumiwa na mawakili wa serikali.

"Licha ya mashauri hayo pia serikali imeendesha mashauri yasiyohusu fedha yenye umuhimu mkubwa kwa ustawi wa taifa letu ikiwemo shauri la mradi wa mafuta ghafi kutoka Hoima-Uganda mpaka Chongoleani-Tanga.

Pia, alisema ofisi hiyo imeshinda shauri la kupinga mkataba wa uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam na shauri la kupinga uwekezaji katika kiwanda cha Saruji Tanga.

Alisema mafunzo hayo yamejikita kwenye maeneo ambayo huzalisha mashauri mengi dhidi ya serikali, ambapo kufikia Aprili 2024 ofisi hiyo iliendesha mashauri 7,813 kati ya mashauri hayo 7,798 yalikuwa ya ndani ya nchi na mashauri 15 yalikuwa nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Dk.Luhende, ofisi hiho iliendesha mashauri mengine 179 kwa kipindi hicho, ambapo mashauri 148 yalikuwa ya ndani ya nchi na mashauri 31 yalikuwa ya nje ya nchi kati ya mashauri hayo yalijikita kwenye masuala ya mikataba ya ujenzi, uwekezaji na taratibu za manunuzi.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini aliwaagiza mawakili hao kwenda kuwa chachu katika kupunguza na kutatua migogoro ya uwekezaji katika sekta ya madini na rasilimali zote nchi.

Pia aliwataka kupunguza idadi ya mashauri ya madai na usuluhishi yanayofunguliwa na yanayoendelea kwa kuyamaliza kwa njia ya usuluhishi, ili kuimarisha juhudi za serikali katika kuwavutia wawekezaji na kutekeleza miradi mbalimbali nchi.

Pia, aliwaagiza kuishauri serikali na taasisi zake kikamilifu namna bora ya kumaliza migogoro na wananchi au wawekezaji bila kuathiri maslahi ya nchi, ikiwa ni pamoja na kuwashauri waajiri kuhusiana na taratibu za uendeshaji wa mashauri pale wanapohitaji kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi wa umma.

Katika hatua nyingine aliwaasa mawakili hao kufuata kanuni za maadili ya utumishi wa umma kwa kuwa na tabia na mienendo inayozingatia utoaji wa huduma bora, utii kwa serikali, utoaji wa huduma bila upendeleo, kufanya kazi kwa uadilifu kuwajibika kwa umma na kuheshimu sheria za nchi.

CamScanner

## 7,813>>Mashauri ya madai yaliyoendeshwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

# Trilioni 1.5/- zaokolewa Ofisi Wakili Mkuu Serikali

**Na LILIAN JOEL**, *Arusha*

WAKILI Mkuu wa Serikali Dk. Boniphace Luhende, amesema ofisi hiyo imeokoa fedha za serikali sh. trilioni 1.5, baada ya kushinda mashauri 15 ya usuluhishi kati ya 19 yaliyofunguliwa ndani na nje ya nchi kati ya Julai mwaka jana hadi Aprili, mwaka huu.

Ilisema kati ya mashauri ya madai 7,813 yaliyoendeshwa na ofisi hiyo, mashauri 762 yalimalizika, ambapo 743 yenye thamani ya sh.bilioni 406.4 serikali ilishinda.

Dk.Luhende alisema hayo jana Jijini Arusha wakati wa mafunzo ya mawakili wa serikali kutoka mashirika na taasisi za serikali.

Mafunzo hayo yalikuwa na kaulimbiu ya 'Uendeshaji wa Mashauri ya Serikali Wajibu wa Majukumu ya Mawakili wa Serikali' yaliyoenda sanjari na uzinduzi wa nembo itakayotumiwa na mawakili wa serikali.

"Serikali iliendesha mashauri yasiyohusu fedha yenye umuhimu mkubwa kwa ustawi wa taifa letu, ikiwemo shauri la mradi wa mafuta ghafi kutoka Hoima-Uganda mpaka Chongoleani-Tanga na kushinda, ambapo mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya shilingi trilioni nane,"alisema.

Pia, alisema ofisi hiyo ilishinda shauri la kupinga mkataba wa uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam na shauri la kupinga uwekezsji kiwanda cha saruji Tanga.

Alisema hadi kufikia Aprili mwaka huu ofisi hiyo iliendesha mashauri 7,813 kati ya mashauri hayo 7,798 yalikuwa ya ndani ya nchi na 15 nje ya nchi.

Dk.Luhende alisema ofisi hiyo iliendesha mashauri mengine 179 ambapo mashauri 148 yalikuwa ya ndani ya nchi na 31 ya nje ya nchi yaliyojikita katika mikataba ya ujenzi, uwekezaji na taratibu za ununuzi.

"Pia ofisi hii imeshughulikia notisi za siku tisini 723 zilizowasilishwa katika kupindi cha Julai mwaka jana hadi Aprili mwaka huu na kwa asilimia kubwa zinahusu ardhi, kazi na mikataba,"alisema.

Awali, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini, aliwaagiza mawakili hao kuwa chachu ya kupunguza na kutatua migogoro ya uwekezaji katika sekta za madini na rasilimali zote nchi.

"Mwaka huu tuna uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani, hizi ni chaguzi muhimu katika nchi yetu. Nendeni mkasimamie na kuendesha vizuri mashauri ya uchaguzi yatakayofunguliwa kabla na baada ya chaguzi hizo,"alisema.

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Alice Mtulo, alisema mafunzo hayo yalishirikisha mawakili zaidi ya 500 wenye hati idhini ya kuendesha mashauri kwa niaba ya ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI**

**Tareho 20/5/2024**

**TANGAZO LA MNADA**

**Halmashauri ya Wilaya ya Rifiji Mkoa wa Pwani Inawatangazia Umma kwamba Itaondosha Magari, Pikipiki, Mitambo na Vigae kwa njia ya mnada wa hadhara. Mnada huo utafanyika katika Ofisi za zamani za Halmashauri ya Rufiji (Utete). Mali zitakazohusika katika mnada huo ni kama inavyoonyeshwa hapa chini;-**

**A: MAGARI**

# Ndani ya Habari

**UCHUMI:** Reli ya SGR itakavyofungua utalii Mikumi **UK 12**

**HABARI:** Mabadiliko ya tabianchi yanavyowakimbiza jamii ya wafugaji **UK 11**

## Korti yaitupa kesi dhidi ya CAG, AG

**Daniel Mjema**, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Dodoma. Mahakama Kuu ya Tanzania imesema kesi ya kikatiba iliyofunguliwa na mwanaharakati Alphonce Lusako dhidi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) akipinga malipo ya Sh7.6 bilioni haina mashiko, hivyo imeitupa.

Kupitia kesi namba 16 ya 2023, Lusako alikuwa akipinga malipo ya fedha hizo zilizotumwa kwa sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza kwa ajili ya kujenga jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza, akisema malipo hayo yalikiuka sheria.

Lusako alimfungulia kesi CAG kama mjibu maombi wa kwanza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) kama mjibu maombi wa pili katika kesi hiyo ambayo ilitolewa hukumu Mei 27, 2024 na Jaji Deo Nangela wa Mahakama Kuu Dodoma.

Katika msingi wa kesi hiyo, Machi 30, 2023, CAG aliwasilisha kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ripoti ya ukaguzi kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2021 ambayo pamoja na mambo mengine, ilionyesha matumizi hayo ya Sh7.697 bilioni.

Mwanaharakati huyo kwa mujibu wa hukumu hiyo, alisema matumizi ya fedha hizo zilizotolewa kutoka mfuko mkuu wa Serikali yalikiuka sheria za nchi, lakini CAG na AG katika majibu yao wakasema, malipo hayo yalifanywa kwa mujibu wa bajeti.

Katika maombi yake, mwanaharakati huyo aliiomba Mahakama itamke kuwa kutolewa kwa fedha hizo kwenda sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza kulikiuka ibara za 136(1)(a), 136(1)(b), 137(6), 143(2)(a) na (b) ya Katiba ya Tanzania.

Aliomba Mahakama itoe tamko utoaji wa fedha hizo kwenda kwa sekretarieti hiyo ulikiuka ibara ya 47(1(a) ya Sheria ya Bajeti ya mwaka 2014.

Pia, aliiomba Mahakama itamke kuwa kitendo cha AG kushindwa kumshauri Rais na Baraza la Mawaziri kwa usahihi kuhusu Katiba na Sheria, alikiuka ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aliiomba Mahakama imwagize CAG ashauri kuchukuliwa hatua kwa wale wote waliohusika na uvunjifu wa Katiba na sheria katika utoaji wa fedha hizo na imwagize CAG kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa amri hiyo ya mahakama.

> **"Kwa msingi huo, Katiba imeweka masharti magumu kuhusu matumizi ya fedha hizo. Hakuna fedha zinaweza kutolewa labda tu kwa ajili ya matumizi yaliyoidhini-shwa na Katiba ya nchi au sheria."**
>
> Alphonce Lusako, mwanaharakati

### Hoja za mdai zilivyokuwa

Jaji Nangela alisema Wakili John Seka alirejea hoja ya mteja wake akiiomba Mahakama kukosoa namna na staili ambayo fedha hizo zilitolewa kutoka mfuko mkuu wa Serikali kwenda kwa Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza.

Mwanaharakati huyo alijenga hoja kuwa, kulingana na ripoti ya CAG, fedha hizo hazikuwa zimetengwa katika bajeti wala kuombwa na sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza, ikizingatiwa kuwa ujenzi huo haukuwa umepangwa katika mwaka huo wa fedha.

Kwa mujibu wa hoja zake, CAG katika ripoti kwa Rais alieleza kutolewa kwa fedha hizo kutekeleza shughuli ambayo haikuwa kwenye bajeti, kunaathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na kutoa mwanya wa ubadhirifu.

Kwa maoni ya mwanaharakati huyo, suala hilo halikupaswa kuishia tu kwa CAG kutoa mapendekezo yake kwa Serikali Kuu, badala yake, hatua kali zilipaswa kuchukuliwa kwa waliohusika, kwani vitendo vyao vilikiuka Katiba ya nchi.

Alieleza kuwa Serikali Kuu na CAG hawakuzingatia utaratibu uliowekwa na Katiba wakati wa kupeleka fedha hizo kwa sekretarieti ya Mwanza, hivyo kuiomba mahakama iyakubali maombi yake na amri ambazo ziliombwa.

CAG na AG kupitia kwa Wakili wa Serikali Mkuu, Hangi Chang'a alisema hoja ya msingi katika kesi hiyo imeegemea katika matumizi mabaya ya fedha za umma, lakini ikasisitiza utoaji wa fedha hizo haukukiuka Katiba wala sheria.

### Hoja za kuamuliwa na Mahakama

Katika kesi hiyo, Mahakama ilibainisha hoja nne ili kuamua mabishano ya mleta maombi na wajibu maombi (CAG na AG) na moja ni kama ripoti ya ukaguzi ya CAG kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2021 inafaa kuaminiwa.

Hoja ya pili ni kama kutolewa kwa fedha hizo kutoka mfuko mkuu wa Serikali kwenda sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza ulifuata kanuni za utoaji fedha kama zilivyoainishwa na vifungu mbalimbali vya Katiba vilivyotajwa na mdai.

Hoja ya tatu ni kama vitendo vya CAG kuhusiana na utoaji wa fedha hizo ulizingatia kifungu cha 47(1)(a) cha sheria ya bajeti, na nne kama kitendo cha kutomshauri vizuri Rais na Baraza la Mawaziri kulikiuka ibara ya 59(3) ya Katiba.

Jaji alisema kwa kuzingatia ofisi ya CAG ni ya kikatiba chini ya ibara ya 143(1), hakuna mtu atatilia shaka uhalisia wa ripoti na zaidi maudhui ya ripoti zake, hivyo hoja ya kwanza inajibiwa kuwa zinaaminika.

Kulingana na Jaji, aliamua kujibu hoja ya pili na ya tatu kwa pamoja akisema kwa mtazamo wake, CAG ana majukumu mawili, moja ikiwa ni kufanya ukaguzi na ya pili fedha zote zinazotolewa zinafuata Katiba ya nchi.

Jaji alisema swali la msingi la kujiuliza ni je, vifungu vya Katiba alivyoviainisha mdai vilikiukwa kama inavyodaiwa, akisema fedha zinazohifadhiwa na kutunzwa katika mfuko mkuu wa Serikali ni fedha za umma.

"Kwa msingi huo, Katiba imeweka masharti magumu kuhusu matumizi ya fedha hizo. Hakuna fedha zinaweza kutolewa labda tu kwa ajili ya matumizi yaliyoidhinishwa na Katiba ya nchi au sheria," alisema Jaji.

"Kama matumizi hayo yameidhinishwa na sheria ya fedha au kwa sheria iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ndiyo ibara ya 136(1(a) na (b) ya Katiba inasema hivyo," alisema.

"Vilevile ibara ya 136(3) ya Katiba inasema hakuna fedha itakayotolewa katika mfuko mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya Serikali, isipokuwa matumizi hayo yamepata idhini kutoka kwa CAG na lazima zitolewe kwa mujibu wa sheria."

Jaji alisema kwa maoni yake anaona anachotoa CAG ni 'Grant of Credit' kwa mlipaji mkuu wa Serikali na lazima awe amepokea maombi kutoka kwa mlipaji mkuu, akasema haoni kosa katika hatua hizo.

Akirejea hoja za mdai, Jaji alisema ni msingi wa kisheria kwa hakuna matumizi yanaweza kufanywa nje ya bajeti ambayo yameidhinishwa na sheria ya fedha ambayo hutungwa na Bunge baada ya kumaliza kupitisha bajeti.

"Katika shauri tulilonalo hakuna ubishi kuwa, wakati CAG anatekeleza jukumu lake la ukaguzi kwa mwaka ulioishia Juni 2021, kwanza alitoa kile alichokibaini na hitimisho kuwa ujenzi wa jengo hilo haukuwa umejumuishwa kwenye bajeti."

Jaji akasema katika hukumu yake kulingana na ripoti ya CAG sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza ilipokea Sh8.33 bilioni kwa ajili ya kazi hiyo na kwamba, sehemu ya fedha hizo, yaani Sh7.697 bilioni ndizo zilitoka Hazina.

"Zaidi ya hilo na kulingana na ripoti ya CAG, fedha hizo alizipa alama kuwa ni 'unbudgeted funds' au fedha ambazo hazikuwepo kwenye bajeti na kupendekeza kuwa kwa siku zijazo, Serikali ihakikishe inazingatia sheria ya bajeti," alisema Jaji.

Alisema hakuna ubishi kuwa katika ripoti hiyo, CAG alinukuliwa akisema kutolewa kwa fedha kutekeleza miradi ambayo haikuwa katika bajeti kunaathiri utekelezaji wa miradi iliyoko kwenye bajeti na inatoa mwanya wa ubadhirifu.

Hata hivyo, Jaji alisema kwa kuwa maoni hayo yalitolewa na CAG na kuibua hoja, lakini ukisoma wasilisho la mdai kuhusu fedha hizo, yeye anashawishika kuwa fedha hizo awali zilikuwa zimepangwa kwa ajili ya matumizi husika.



# Serikali yaokoa tril 1.5/- mashauri mahakamani

**Na Veronica Mheta, Arusha**

SERIKALI imeokoa Sh trilioni 1.5 baada ya kushinda mashauri 15 ya usuluhishi kati ya 19 yaliyokuwa yamefunguliwa ndani na nje ya nchi katika kipindi cha Julai mwaka jana hadi Aprili mwaka huu.

Aidha, kati ya mashauri ya madai 7,813 yaliyoendeshwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Julai mwaka 2023 hadi Aprili mwaka 2024, mashauri 762 yalimalizika. Mashauri 743 yenye thamani ya Sh bilioni 406.4 yalimalizika kwa ushindi upande wa serikali.

Wakili Mkuu wa Serikali, Dk Boniphace Luhende alisema hayo Arusha jana wakati wa mafunzo ya siku tatu ya mawakili wa serikali yenye kaulimbiu: 'Uendeshaji wa mashauri ya serikali wajibu wa majukumu ya mawakili wa serikali', yaliyoenda sanjari na uzinduzi wa nembo itakayotumiwa na mawakili wa serikali.

Dk Luhende alisema ofisi hiyo imeshinda shauri la kupinga mkataba wa uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam na shauri la kupinga uwekezaji katika Kiwanda cha Saruji Tanga katika kipindi hicho cha Julai hadi Aprili, mwaka huu.

Alisema mafunzo hayo yamejikita kwenye maeneo ambayo huzalisha mashauri mengi dhidi ya serikali.

Hadi Aprili mwaka 2024, ofisi hiyo iliendesha mashauri 7,813 na kati ya hayo, 7,798 yalikuwa ya ndani ya nchi na 15 yalikuwa nje ya nchi.

Kwa mujibu wa Dk Luhende, ofisi hiyo iliendesha mashauri mengine 179 kwa kipindi hicho ambacho 148 yalikuwa ya ndani ya nchi na mashauri 31 yalikuwa ya nje ya nchi.

Mashauri hayo yalijikita kwenye masuala ya mikataba ya ujenzi, uwekezaji na taratibu za ununuzi.

"Pia ofisi hii imeshughulikia notisi za siku tisini 723 zilizowasilishwa katika kipindi cha Julai mwaka jana hadi Aprili mwaka huu, ambazo kwa asilimia kubwa ya notisi hizo zinahusu masuala ya ardhi, kazi na mikataba," alisema.

Akifungua mafunzo hayo, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Jumanne Sagini aliwasihi mawakili kuwa chachu katika kutatua migogoro ya uwekezaji katika sekta ya madini na rasilimali zote nchini.

Alitaja maagizo mengine kuwa ni pamoja na kupunguza idadi ya mashauri ya madai na usuluhishi yanayofunguliwa na yanayoendelea kwa kuyamaliza kwa njia ya usuluhishi ili kuimarisha juhudi za serikali katika kuvutia wawekezaji na kutekeleza miradi mbalimbali nchini.

"Huu mwaka tuna uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani, hizi ni chaguzi muhimu katika nchi yetu. Nendeni mkasimamie na kuendesha vizuri mashauri ya uchaguzi yatakayofunguliwa kabla na baada ya uchaguzi," alisema.

Aliwaasa mawakili hao kuishauri vema serikali na taasisi zake namna bora ya kumaliza migogoro na wananchi au wawekezaji bila kuathiri maslahi ya nchi, ikiwa ni pamoja na kuwashauri waajiri ipasavyo kuhusiana na taratibu za uendesha wa mashauri wanapohitaji kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watumishi wa umma.

Pia aliwaasa mawakili kufuata kanuni za maadili ya utumishi wa umma kwa kuwa na tabia na mienendo inayozingatia utoaji wa huduma bora, utoaji wa huduma bila upendeleo, kufanya kazi kwa uadilifu, kuwajibika kwa umma na kuheshimu sheria za nchi.

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Alice Mtulo alisema mafunzo hayo yameshirikisha mawakili zaidi ya 500 kutoka taasisi 114 zenye hati idhini ya kuendesha mashauri kwa niaba ya ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Yalishirikisha pia wakufunzi wabobezi wakiwamo majaji wastaafu ambao wanatoa mada mbalimbali.

Mada hizo ni; marekebisho ya sheria ya uchaguzi na matokeo yake, utaratibu na utatuzi wa migogoro itokanayo na mikataba ya uwekezaji baina ya nchi na nchi, utaratibu wa utatuzi wa migogoro ya madini na maliasili za nchi na uchambuzi wa kanuni za Mahakama ya Rufani ya Tanzania za mwaka 2024.

CamScanner